KISWAHILI ACTIVITIES GREDI 1

1.

1. **UFAHAMU** (Alama 10)
   Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata: (Alama 5)
   Maria na Asha walikuwa marafiki. Walipendana sana. Walienda shuleni pamoja. Walikuwa watoto wenye heshima na wenye bidii sana. Walimu waliwapenda kwa tabia zao nzuri.

   a. Ni nani walikuwa marafiki? (alama 2)

   b. Walikuwa na tabia gani? (alama 1)

   c. Ni nani aliwapenda? (alama 1)

   d. Walienda wapi pamoja? (alama 1)

2. Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali (alama 5)
   Tom aliamka saa moja asubuhi. Alimpata Joan akinywa chai. Joan alimwambia Tom achukue kikombe jikoni ili anywe chai. Baada ya kupata kiamshakinywa walienda nje kucheza. Hawakuwa waende shuleni maana ilikuwa siku ya Jumamosi.

   a. Tom aliamka saa ngapi?

   b. Joan alikuwa anafanya nini?

   c. Tom alipata kikombe wapi?

   d. Baada ya kiamshakinywa walienda wapi?

   e. Kwa nini hawakuenda shuleni?

2. SARUFI (alama 20)

   1. Tenganisha silabi

      a. Maua =

      b. Pole =

      c. Dawati =

      d. Kiti =

      e. Moja =